

Tunafurahia hali nzuri ya hewa na hali ya maisha nzuri hapa Queensland. Hata hivyo, majanga ya kimaumbile kama vile tufani, dhuruba na mafuriko ni sehemu isiyoepuka katika mazingira yetu. Historia imeonyesha kwamba hatuwezi kunyamaza hatari hizi zinazoletwa na majanga kama haya.

Chukua muda Sasa ili kujitayarishia mpango wako wa dharura kwa:

- Kutayarisha Mpango wako wa Dharura;
- Kutayarisha Mkoba wako wa Dharura,
- Kutayarisha nyumbani pako; na
- Kusikiliza onyo

Kazi hizi rahisi zinaweza kukusaidia kukutayarishia, kuishi, na kukupunguzia athari za majanga ya kimaumbile.

Zifuatazo ni hatua nne za kukusaidia kujitayarishia Mpango wako wa Dharura:

1. Fanya utafiti kuhusu hatari na mipangilio ya usimamizi wa majanga katika jumua yako.

- Ni hatari zipi ambazo zitaathiri jumua yako? Je kuna taarifa yoyote kuhusu Mipango ya Usimamizi wa Janga kwa hatari hizi?
 - Angalia kwenye maktaba yako yaliyo karibu nawe na baraza lililo karibu nawe kwa taarifa na mipango.
 - Angalia baraza lako lililo karibu nawe kuhusu mifumo ya onyo iliyo karibu nawe, mchakato wa kutolewa na njia za kutolewa zilizoteuliwa.
- Uliza kuhusu mipango yako ya dharura na mipango yako ya kutolewa katika mahali pako pa kazi, shule na watoaji huduma ya utunzaji watoto. Angalia kama wanataka maelezo ya mawasiliano ya dharura ya familia yako.
- Msaada wako ulio karibu nawe na familia yako ni upi wakati wa dharura?
 - Ulizia maelezo ya mawasiliano ya mawakala ya msaada ulio karibu nawe na uweke kumbukumbu ya mawasiliano haya katika Mpango wa Dharura.
 - Kama familia yako itahitaji msaada wa kutolewa, pata kujua zaidi kuhusu msaada unaoweza kupatikana kwenye baraza lililo karibu nawe na wakala wa msaada.
- Jizoeshé na hali za hewa zinazotolewa na Biuro ya Meteorolojia (www.bom.gov.au na huduma za simu).

2. Zungumzia sehemu zinazowezezana pamoja na miitikio na familia yako.

- Zungumza kila hatari na sehemu zinazowezezana.
- Ungeweza kufanya nini katika kila tukio la dharura?
- Uenda ukawa wapi endapo dharura itatokea?
- Kutegemea na dharura, amua namna ambavyo ungewasiliana na ni wapi ungekutana.
- Je, kila mtu anajua Ishara ya Onyo ya Dharura ya Wastani (SEWS) na nini kinahitajika kufanywa wakati onyo hii itakapotolewa? Ili kujifunza zaidi kuhusu SEWS tembelea www.disaster.qld.gov.au
- Je, kila mtu anajua kusikiliza katika kituo chako cha redio kilicho karibu nawe ili kusikiliza habari na onyo?
- Huenda ukahitajika pia kujitayarishia kutolewa. Zungumzia ni wapi utakapoenda endapo hutaweza kurudi nyumbani au kama utalazimika kutoka nyumbani pako.
- Teua sehemu mbili za kukutania endapo kutakuwa na dharura, moja ikiwa karibu na nyumbani pako na nyingine ikiwa nje ya ujirani wako ambayo inaweza kufikiwa na kila mtu kwa urahisi.
- Teua wanafamilia wawili au rafiki wasioishi nawe (mmoja katika eneo lako na mwingine nje ya eneo lako) kuwa wakufikishiwa mawasiliano ya dharura na familia endapo wewe na familia yako mtatengana. Hakikisha kwamba wanafamilia wote wanajua namna ya kuwasiliana na watu hawa.
- Zungumzia hali za kimatibabu za wanafamilia. Jumuisha dawa muhimu na vipimo katika Mkoba wako wa Dharura
- Zungumzia ni mahitaji yapi ya matayarisho yanafaa kufanyiwa wanyama wapenzi wako

3. Rekodi maelezo muhimu katika Mpango wako wa Dharura, kama vile:

- Nambari za simu za dharura na za husika: Sufuri Mara Tatu (000); 132 500 (SES); huduma za kimatibabu; baraza lililo karibu nawe; watoaji huduma wa umeme na wengine; watoaji huduma wa bima; watu wa ukoo na marafiki katika Mpango wako wa Dharura
- Simu za mkononi za wanafamilia wote, nambari nyingine kama vile kazini, shuleni, watoaji huduma wa utunzaji wa mtoto, marafiki, majirani na nambari za mawasiliano ya dharura ya familia.
- Maelezo ya sehemu mbili za kukutania ambazo umeteua.
- Hali zozote mahuksusi za kimatibabu, dawa muhimu na vipimo.
- Maelezo ya wanyama wako – mafafanuzi, picha, maelezo ya mawasiliano ya daktari wa mifugo, dawa.
- Mitabedi ya redio katika kituo chako cha redio kilicho karibu nawe (www.abc.net.au/local), tovuti ya Biuro ya Meteorolojia (www.bom.gov.au) na huduma za hali ya hewa za simu kwa onyo zilizokaribu nawe.

4. Hakikisha kwamba kila mtu katika nyumba yako amejitayarisha.

- Tayarisha Mkoba wa Dharura na uifadhi mahali salama, panapoweza kufikika.
- Hakikisha na ufanyie mazoezi ya Mpango wako wa Dharura mara kwa mara (mara tatu kwa mwaka).
- Wafunze watoto namna ambavyo wanaweza kupiga simu Sufuri Mara Tatu (000) katika wakati wa dharura (tumia nambari 112 kutoka kwenye simu za mkononi). Piga simu pekee Sufuri Mara Tatu (000) kama unaamini kwamba dharura hiyo inatishia maisha, ni muhimu sana na inahitajika.
- Hakikisha kwamba wanafamilia wanao uidhiishwaji wa sasa wa Huduma ya Kwanza. Jumuisha Mkoba wa Huduma ya Kwanza ambao una kila kitu katika Mkoba wako wa Dharura. Utoaji mafunzo na mitambo ya Huduma ya Kwanza unatolewa na Huduma za Ambulensi za Queensland (www.ambulance.qld.gov.au).
- Hakikisha ya kwamba kila mtu anajua namna ya kusikiliza katika onyo.
- Undaa kadi za dharura za pochi kwa wanafamilia wote kuweza kurejelea wakati wanapoamiliha Mpango wako wa Dharura.
- Hakikisha kwamba kila mtu anajua ni wapi, vipi na lini wanazima swichi kuu ya umeme, maji na

gesi endapo kutakuwa na kutolewa.

- Onyesha Mpango wako wa Dharura katika friji au kibao arifa ya familia, toa nakala za wanafamilia, wa marafiki wanaofaa, familia na majirani na uhifadhi nakala katika Mkoba wako wa Dharura.
- Fikiria kujiunga na shirika la huduma ya dharura ya jumuiya kama vile Huduma ya Dharura ya Serikali (SES) ili kujifunza zaidi na kusaidia jumuiya yako kujitayarishia na kuitikia majanga ya kimaumbile (www.emergency.qld.gov.au/ses).

siku zote kumbuka

Husisha wanafamilia wote katika matayarisho yako ya janga ili wote waweze kuelewa hatari na hatua zinazofaa kuchukuliwa na zinazohitajika wakati kwa dharura

Kuwa na Mpango wa Dharura ni hatua muhimu katika kutayarisha familia yako kujitayarisha, kuishi na kukabiliana na dharura zitakazotokea.

Wanafamilia wote wanahitaji kujua ni wapi ambapo Mpango wa Dharura unawekwa.

Fanyia mazoezi Mpango wako wa Dharura pamoja na wanafamilia wote kila baada ya miezi michahe ili kuhakikisha kwamba kila mtu anajua ni nini cha kufanya endapo dharura itatokea.

Broshua hii ni ya taarifa pekee na imetolewa kwa roho safi. Idara ya Usalama wa Jumua, Usimamizi wa Dharura wa Queensland na Huduma ya Dharura ya Serikali yote haitawajibika mtu yeyote kwa mujibu wa kupoteza au kuharibika kokote (kukiwemo athari ya kupoteza au kuharibu) ambayo kunaweza kupatikana na kutozwa, au kunakoweza kutokea moja kwa moja au vinginevyo, kwa mujibu wa kutegemea wa mtu yeyote katika taarifa ilimo kwenye broshua hii.

© 2013 Department of Community Safety

Kwa taarifa zaidi kuhusu kujitayarishia dharura tembelea www.disaster.qld.gov.au

Mpango wa Dharura



Maelezo ya Mawasiliano ya Familia

Jina	Nambari ya Simu	Anwani ya baruapepe

Sehemu za kukutania endapo mtatengana au mtahitajika kutolewa

Mahali pa kukutana palipo karibu	
Anwani	
Nambari ya simu	
Anwani ya baruapepe	
Mahali pa kukutana palipo mbali kidogo	
Anwani	
Nambari ya simu ya mawasiliano	
Anwani ya baruapepe	

Mawasiliano ya Dharura ya Familia Yalioteuliwa

Jina la mwasiliani aliyekaribu	
Anwani	
Nambari za simu za nyumbani / kazini	
Nambari ya simu ya mkononi	
Anwani ya baruapepe	
Jina la mwasiliani aliye nje-ya-mji	
Anwani	
Nambari za simu za nyumbani / kazini	
Nambari ya simu ya mkononi	
Anwani ya baruapepe	

Ugamvi wa Huduma Kuu – namna ya kuzima ugamvi huo na mahali hapo

Umeme		
Gesi		
Maji		

Nambari muhimu za simu

Polisi, Moto na Ambulensi	000 Sufuri Mara Tatu (112 kutoka kwenye simu ya mkononi)
Huduma za Dharura za Serikali (SES)	132 500
Halmashauri ya eneo lako	
Mtoaji huduma wa umeme	
GP iliyokaribu nawe au vituo vya daktari	
Hospitali	
Daktari wa matibabu ya mifugo	
Mtoaji bima	
Mtoaji huduma za utunzaji wa watoto	
Shule za msingi za eneo lako	
Shule za upili za eneo lako	
Eneokazi	
Eneokazi	
Huduma ya simu ya Biuro ya Meteorolojia (http://www.bom.gov.au/other/voice.shtml)	
Rafiki	
Rafiki	
Majirani	
Majirani	

Taarifa za kimatibabu

Matibabu	Nani anahitaji na kipimo kipi?

Ni wapi ambapo utazihifadhi endapo tunaishi kwenye nyumba? Wanyama wapenzi wetu watahifadhiwa wapi?

Tarehe za mazoezi ya Mpango wa Dharura (mara tatu kwa mwaka):

- _____ Mitabendi ya kituo cha redio kilicho karibu nawe:
- _____
- _____